# MAJI TANZANIA

TOLEO NA 029

JULAI - SEPTEMBA, 2025


# DKT. SAMIA ATAMBULIKA KUWA KINARA KATIKA HUDUMA YA MAJI KWA TUZO YA JUU YA KIMATAIFA



# DKT. SAMIA ATAMBULIKA KUWA KINARA KATIKA HUDUMA YA MAJI KWA TUZO YA JUU YA KIMATAIFA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ametunukiwa Tuzo ya Rais ya Kimataifa ya Wabunifu wa Mabadiliko katika Sekta ya Maji 2025 (Presidential Global Water Changemakers Award 2025), heshima kubwa inayotolewa na taasisi ya maji duniani, ( Global Water Partnership) kwa ushirikiano na Umoja wa Afrika.

Tuzo hiyo imetolewa rasmi na Rais Duma Boko wa Jamhuri ya Botswana, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tuzo za Rais za Kimataifa za Wabunifu wa Mabadiliko katika Sekta ya Maji 2025, ambapo kwa niaba ya Rais Dkr. Samia, tuzo ilipokelewa na Balozi James Bwana, Balozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini.

Tuzo imetolewa wakati wa Mkutano wa Kilele wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji wa AU-AIP 2025, ulioanza jijini Cape Town, Afrika Kusini, na unatarajiwa kumalizika tarehe 15 Agosti 2025.

Global Water Partnership imetambua uongozi bora na jitihada za mageuzi za Rais Samia katika sekta ya maji, ikiwemo uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya maji, upanuzi wa huduma ya maji safi kote





katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na mikakati bunifu ya ufadhili kama vile hati fungani ya Kijani (Green Bond) lililotolewa na Mamlaka ya Maji ya Tanga chini ya Wizara ya Maji

# Aweso aitaka RUWASA kufikisha huduma ya maji Vijiji vyote nchini









Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ametoa wito kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kufikisha huduma ya majisafi ya bomba katika vijiji takribani 1,500 vilivyobaki ifikapo mwaka 2030 ili huduma hiyo ipatikane katika vijiji vyote 11,353 vinavyopaswa kuhudumiwa na Wakala huyo hapa nchini, ambapo hadi sasa jumla ya vijijini 9,894 zimefikiwa na huduma hiyo.

Ametoa wito huo Mkoani Dar es Salaam wakati akifunga kongamano la siku tano la tathimini ya RUWASA iliyofanywa na Menejimenti ya Wakala huyo ikijumuisha Mameneja wa Mikoa na kuhudhuriwa na baadhi ya wadau wake.

Waziri Aweso pia alipongeza eneo la Utoaji huduma ya Maji Vijijini linalosimamiwa na RUWASA kupitia Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSO) kuwa linafanya vizuri huku ukitaka nguvu zaidi ili huduma iwe endelevu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya RUWASA Mha. Ruth Koya aliishukuru Wizara ya Maji kwa kuiwekea taasisi hiyo mazingira rafiki ya kufanyia kazi hali inayosaidia utendaji wake kuwa rahisi na kupata matokeo ya haraka katika kuwahudumia wakazi wa vijijini huduma muhimu ya majisafi na salama.

Awali, akitoa maelezo kwa mgeni rasmi kuhusu kongamano hilo, Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA Mha. Wolta Kirita alisema katika siku tano za kongamano hilo la kujitathimini kumekuwa na mijadala ya kina kuhusu utendaji kazi wa miaka sita tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo Julai 1, 2025 na kwamba mwelekeo wa sasa ni kuimarisha zaidi eneo la usambazaji maji kwani lengo la kuanzishwa kwake ni kutoa huduma ya majisafi kwa wakazi wa maeneo ya vijijini Tanzania Bara.

Katika hatua nyingine, RUWASA imempatia zawadi ya tuzo maalum Waziri Aweso kama shukrani na kumbukumbu kwa huduma yake bora kwa taasisi hiyo na sekta ya maji kwa ujumla. Kikao na hafla ya tuzo imefanyika mapema Agosti 2025.

# Waziri Aweso awapa heko timu Maji kwa ushindi wa Michezo SHIMIWI





Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameipongeza timu ya michezo ya Wizara ya Maji (Maji Sport) kwa ushindi walioupata katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) Jijini Mwanza.

Pongezi hizo amezitoa kwa njia ya simu kutokea Pangani mkoa wa Tanga baada ya timu hiyo kufika ofisini kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Maji kumkabidhi vikombe vinne vya ushindi vilivyopatikana katika mashindano hayo.

Vikombe hivyo ni kikombe cha mshindi wa kwanza mchezo wa mishale (Darts) na Mchezo wa Draft, wote wanaume. Mshindi wa kwanza Karata na mshindi wa pili Bao kwa timu ya wanawake.

Amesema ushindi huo ni heshima kwa Wizara ya Maji na uthibitisho kuwa kila jambo linaloihusu Wizara ya Maji linazingatiwa kama shughuli maalumu na kupewa kipaumbele cha maandalizi.

Aidha, ameahidi kutoa zawadi ya shilingi milioni tano kwa ushindi huo.

Naye katibu Mkuu wa Wizara Mhandisi Mwajuma Waziri amesema yeye binafsi amefurahishwa na ushindi huo.

Amesema mwisho wa mchezo huo ni maandalizi kwa michezo mingine kwa mwaka 2026.

# Katibu Mkuu Maji amtaka mkandarasi kufanya kazi saa 24 kukamilisha mradi Tanga

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amemtaka Mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji wa Miji 28 katika miji ya Korogwe, Handeni, Muheza na Pangani kufanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha haraka utekelezaji wa mradi.

Ametoa maelekezo hayo wakati akikagua mradi huo.

Amesema hali ya utekelezaji wa mradi inaridhisha lakini bado mkandarasi anapaswa kuongeza nguvu katika ujenzi ikiwamo eneo la mtambo wa kuchuja maji kwani hakuna changamoto yoyote ya eneo hilo.

Mradi huo unatarajia kuzalisha lita milioni 51 kwa siku, na umefika asilimia 70 ya utekelezaji ukitarajiwa kukamilika Desemba 2025.

Amesisitiza kuwa agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati hivyo Wizara ya Maji haitakuwa na nafasi ya kuongeza muda wa utekelezaji.

Mradi wa maji wa Miji 28 katika Mji wa Korogwe, Handeni Muheza na Pangani unatumia chanzo cha maji kutoka mto Pangani na ni moja ya hatua muhimu ya utekelezaji wa gridi ya taifa ya maji ambayo inalenga kutumia vyanzo vya uhakika vya maji.





# Bodi ya RUWASA Yataka Usimamizi Mzuri Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Ruth Koya, ameelekeza Mameneja wa RUWASA wa Mikoa na Wilaya nchini kusimamia vizuri Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) ili kuimarisha huduma ya maji vijijini na kuwa na uwezo wa kuhudumia maeneo makubwa zaidi.

Amesema viongozi na watumishi wa RUWASA, hususan wa ngazi ya mikoa na wilaya, wanapaswa kubadili mtazamo kutoka kufikiria zaidi ujenzi wa miradi pekee na badala yake kuweka mkazo katika usimamizi wa CBWSOs, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya majisafi na salama.

"Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, imewekeza fedha nyingi katika miradi ya maji kwa lengo la kumtua mama ndoo kichwani, hivyo ni jukumu la viongozi wa RUWASA kuhakikisha huduma hizo zinawafikia wananchi kama ilivyokusudiwa", Mhandisi Koya amebainisha.

Mhandisi Koya ametoa maelekezo hayo katika ziara ya kikazi ya Bodi ya Wakurugenzi ya RUWASA katika Halmashauri ya Msalala katika Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga. Ziara iliyohusisha pia kikao cha kazi na CBWSO tatu za Ilogi, Fufumo na Bulyanhulu.

Bodi ilipokea na kujadili taarifa za utendaji kazi wa CBWSOs hizo, ikiwemo mafanikio na changamoto mbalimbali, kisha ikatoa ushauri wa hatua za kuchukua ili kuboresha zaidi huduma ya maji katika maeneo yao.







Katika kikao hicho Bodi ya Wakurugenzi ya RUWASA iliambatana na Menejimenti ya RUWASA ikiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Mhandisi Wolta Kirita, ambaye pia ni Katibu wa Bodi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 iliyoanzisha RUWASA, wakala hiyo ina jukumu la kuviwezesha, kuvijengea uwezo na kuvisimamia CBWSOs ili viwe na ufanisi katika utoaji wa huduma na kuhakikisha wananchi wa vijijini wanapata majisafi na salama kwa mujibu wa sheria.




# Visima majimboni sasa asilimia 85 Nyang’hwale

Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Nyang’hwale katika kazi ya kuchimba visima imefika asilimia 85 ya utekelezaji.

Lengo la kazi hiyo ni kupunguza adha ya maji kwa wananchi

Programu ya visima 900 inatekeleza mradi wa maji wa visima vitano vya jimbo katika vijiji vitano ambavyo ni Kanegele, Mwingiro, Shabaka, Wavu na Lubando na kuongeza upatikanaji wa maji kufikia asilimia 77.4.

Kaimu Meneja wa RUWASA wa wilaya hiyo Mhandisi Suzan Gogadi ametoa taarifa hiyo kwa viongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2025 wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi wa mradi wa visima vitano kijijini Shabaka.

“Wananchi takribani 5,000 waishio katika vijiji hivyo watapata huduma ya maji safi na salama hivyo kupunguza magonjwa ya milipuko”, Suzan amesema.

Amesema vyanzo vya maji katika mradi ni visima virefu vitano vyenye uwezo wa kuzalisha jumla ya lita 21,150 kwa saa ambapo mkataba wa ujenzi ulianza Januari 06, 2025 na unatarajiwa kukamilika Septemba 30, 2025.

Mradi huo unatekelezwa kwa mfumo wa Force Account na kwa kutumia mafundi wa ndani ambapo gharama za utekelezaji mradi huo ni shilingi milioni 327.

“Hadi sasa jumla ya kiasi cha shilingi milioni 137.15 kimelipwa kwa ajili ya shughuli ya ufungaji wa mfumo wa kutumia nishati ya jua, pampu, ununuzi wa matenki na malipo ya mafundi.

“Chanzo cha fedha za mradi huu ni kupitia Programu ya Malipo kwa Matokeo (PforR) na Fedha Maalum (Special Fund)”, amesema Mhandisi Suzan.




Mkuu wa wilaya ya Nyang’hwale, Grace Kingalame amekiri kuwa uchimbaji wa visima virefu majimboni ni msaada mkubwa katika kuboresha huduma ya maji safi na salama.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2025, Isimail Alli Ussi amesema mradi visima majimboni ni juhudi za serikali kukabili tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama hivyo usimamizi thabiti unahitajika.

# Watumishi wenye sifa waingizwe katika mfumo wa E Utumishi



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Juma Mkomi amewataka wakuu wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ,wakuu wa idara ya rasilimali watu ,pamoja maafisa rasilimali watu kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi kuhakikisha watumishi wote wenye sifa wanaingizwa kwenye mfumo wa (E-utumishi ) na endapo kuna changamoto zozote zitafutiwe ufumbuzi .

Ameyasema hayo wakati akizindua kikao kazi kilicho wakutanisha wakuu wa mamlaka za maji ,wakuu wa idara ya rasilimali watu,pamoja na maafisa rasilimali watu. Kikao kimefanyika katika ukumbi wa Wizara ya Maji, Mtumba jijini Dodoma.

Amewaelekeza wakuu wa mamlaka za maji kufanya tathmini ya mahitaji ya watumishi kupitia mfumo wa Tathmini ya Rasilimali watu ilikufahamu mahitaji ya watumishi wanao hitajika katika taasisi zao.

“Ni muhimu Kuzingatia sera za utumishi na taratibu za ajira zinazo simamia utaratibu ili kuhakikisha kila mtu anatendewa haki katika utumishi wa umma” Mkomi amesema.

Pia amewataka wakuu wa idara pamoja na maafisa rasilimali watu kutokuwa kikwazo katika masuala yanayohusu watumishi kwenye taasisi zao na badala yake wawe daraja la kuwahudumia watumishi.

Akimkaribisha mgeni rasmi Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amesema Wizara ya Maji inaendelea kutoa huduma za kufikisha maji kwa wananchi kupitia taasisi zake na ili kufanikisha hilo wizara inahitajia rasilimali watu ambao watafanya kazi kwa weledi.

Kikao kazi hicho cha siku nne kimelenga kupata mafunzo ya namna bora ya utumiaji wa mifumo ya kiutumishi na utawala.





# Serikali imejipanga kutoa suluhu ya changamoto ya maji Karatu na Monduli.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mhandisi Mwajuma Waziri amesema Serikali itachukua hatua za haraka na za muda mrefu kuondosha upungufu wa huduma ya maji katika maeneo hayo.

Ameielekeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu (KARUWASA) kuhakikisha inafufua kisima cha Bwawani ili kuongeza upatikanaji wa maji na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 66 ya sasa na kufika asilimia 77.



“Katika mpango wa muda mfupi nitatuma Wataalam kuhakikisha kisima moja wapo kilichozingirwa na maji katika eneo la bwawani ambacho hakitumiki kwa sasa kinafufuliwa na kuanza kutumika ili kisaidiane na visima vilivyopo kuongeza uzalishaji”, Mha. Mwajuma amesema.

Aidha, ameongeza kuwa Wataalam wa Wilaya ya Karatu kwa kushirikiana na timu ya wataalamu atakayoituma watafanya utafiti wa maji ardhini kwa ili kuchimba visima vingine zaidi ili kuongeza uzalishaji wa maji kuhudumia wananchi wa Karatu mjini, hatua inayolenga kufikisha upatikanaji wa maji kwa asilimia 85 vijijini na 95 mijini ifikapo mwishoni mwa mwaka 2025, kama Serikali ilivyopanga.



Aidha, kwa upande wa kijiji cha Kansay amewaelekeza Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingara Wizara ya Maji pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuhakikisha pampu iliyopata hitilafu inapata mbadala wake na kuhakikisha huduma ya maji inarejea katika kijiji hicho.

Akiwa Wilayani Monduli, Mhandisi Mwajuma amekagua utekelezaji wa mradi mkubwa wa kutoa maji katika tanki la Ngaramtoni Jijini Arusha kwenda Mji wa Monduli na vijiji 13, unaotekelezwa na Mkandarasi kampuni ya Jandu Plumber kwa gharama ya shilingi Bilioni 20.3. Mradi huo utanufaisha zaidi ya wananchi elfu 57 na upo katika hatua za awali za utekelezaji.

Ametoa wito kwa watumishi wa sekta ya maji katika wilaya hizo kufanya kazi kwa bidii, weledi na uaminifu, na kushirikiana na wananchi kuhakikisha miradi inakuwa endelevu.



# Tanzania na Kenya waungana kuotesha miti kulinda Mto Mara

Nchi ya Tanzania na Kenya zimeshirikiana katika kazi ya uhifadhi katika bonde la mto Mara.

Mkuu wa Wilaya ya Butiama Mhe. Thecla Mkuchika amewaongoza wadau wa bonde la Mto Mara kutoka Tanzania na Kenya katika zoezi hilo la kuotesha miti rafiki wa maji na kusimika vigingi vya mpaka wa Mto katika Kijiji cha Kirumi wilayani Butiama mkoa wa Mara.

Kazi imefanyika ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Mto Mara 2025.
Mto Mara unaanzia milima ya Mau nchini Kenya hadi ziwa Victoria nchini Tanzania.
Amesema zoezi la kuotesha miti na ulinzi wa mto linapaswa kuwa endelevu kwa kila mwananchi anayekaa katika bonde la Mto Mara kutokana na umuhumu wa mto huo kwa jamii inayouzunguka.
Aidha amemuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, Aziza Baruti kuhakikisha anasimamia kuhakikisha miti hiyo inatunzwa. Pia kuhakikisha wakulima na wafugaji wanazingatia sheria inayowataka kufanya kazi zao nje ya eneo la hifadhi ya mto.

Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria Dkt. Renatus Shinhu amesema miti iliyooteshwa kwa siku ya leo ni miti 3,000 huku zoezi likiendela ili kufikisha miti 8000. Amesema Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha Bonde hilo linaendelezwa na kwamba hawatasita kuchukua hatua kwa mtu yeyote anayeharibu bonde hilo.

Naye Mwakilishi kutoka Kenya, Galfen Omuse amesema



Mto Mara umekuwa sehemu ya kuyaunganisha mataifa ya Tanzania na Kenya katika ushirikiano. Ameishukuru serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuonesha nia ya dhati ya kuhakikisha mto mara unatunzwa na kuendelezwa.

Maadhimisho ya Siku ya Mto Mara yamekuwa yakifanyika kila mwaka kwa kupokezana kati ya Tanzania na Kenya yakilenga kushirikishana njia mbalimbali za kuhakikisha mto Mara unatunzwa na kuendelezwa na faida ya pande mbili za nchi

# Tanzania na Kenya kuandaa pamoja kongamano la Bonde la Mto Mara






Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri ametoa wito kwa Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia kilichoko Wilayani Butiama Mkoani Mara na Chuo Kikuu cha Masai-Mara kilichoko nchini Kenya kuandaa kwa pamoja chini ya Uratibu wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria Kongamano la Kisayansi la 15 la Bonde la Mto Mara kwa mwaka 2026.

Wito huo ameutoa wakati akifungua Kongamano la 14 la Kisayansi la Bonde la Mto Mara katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia mjini Butiama mkoani Mara.

Kongamano hilo limehudhuriwa na wadau mbalimbali kutoka Kenya na Tanzania wakiwemo wawakilishi kutoka Chuo Kikuu cha Maasai Mara cha Kenya pamoja na Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia

Amesisitiza kuwa uhusiano kati ya Tanzania na Kenya umekuwa wa muda mrefu na yamezalisha matunda mbalimbali ikiwemo ulinzi wa mto Mara ambao unaanzia milima ya Mau nchini Kenya hadi ziwa Victoria nchini Tanzania

Amesema jitihada za pamoja zitawezesha kupatikana wafadhili wa kudumu ambao watasaidia kuendeleza jitihada za viongozi wa nchi mbili za Kenya na Tanzania katika kupata suluhisho la changamoto zinazolikumba bonde la Mto Mara

Mhandisi Mwajuma amesema hana mashaka na utendaji mzuri wa Chuo cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere na ametoa wito maalum kwa Chuo hicho kuchangamkia fursa aliyoitambulisha kwa jina la Mara Valley Development Project ambayo inahusisha ujenzi wa Bwawa la Borenga katika vijiji vya Borenga na Mrito kwa ajili ya kilimo na matumizi mengine.

“Mradi huo umeandaliwa, unahitaji fedha za kuendeleza. Kwa kuwa hiki ni Chuo cha Kilimo na mradi uko hapa ndani ya mkoa, pokeeni fursa hiyo.” Mhandisi Mwajuma amesema.

Aidha katika kongamano la 14 Mhandisi Mwajuma amewataka Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia, Chuo Kikuu cha Masai-Mara na Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria chini ya uratibu wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria wahakikishe wanaandaa andiko la Mradi wa Kuhifadhi Bonde la Mto Mara.

Maadhimisho ya 14 ya Bonde la Mto Mara kwa mwaka 2025 yanafanyika chini ya kaulimbiu isemayo Hifadhi Mto mara, Tunza Uhai

# BURIANI MHE. NDUGAI




Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri akijumuika na viongozi na wananchi katika Viwanja vya Bunge jijini Dodoma katika ibada maalaum ya kumuaga aliyewahi kuwa Spika wa Bunge la Tanzania na Mbunge wa Kongwa Mkoani Dodoma Hayati Mhe. Job Ndugai (Mb).

Viongozi na wananchi walioshiriki Ibada hiyo wameongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.



# RAIS MSTAAFU MHE. JAKAYA KIKWETE ASHIRIKI MKUTANO MKUU UWEKEZAJI WA MAJI - AFRIKA YA KUSINI




Rais Mstaafu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ameshiriki katika Mkutano Mkuu wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji Barani Afrika unaondelea Jijini Cape Town, Afrika Kusini.

Ameshiriki kwa nafasi yake ya Mwenyekiti Mwenza Msaidizi wa Jopo la Ngazi ya Juu la Programu ya Uwekezaji wà Maji Barani Afrika (the High Level Panel on the Africa Water Investment Programme (AIP).

Mkutano umeandaliwa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika kwa kushirikiana na Serikali ya Afrika Kusini na Jopo la Ngazi ya Juu la Programu ya Uwekezaji wà Maji Afrika (AIP).

Jopo hilo lina Wenyeviti Wenza Watatu ambao ni Rais wa Namibia, Rais wa Senegal na Waziri Mkuu wa Uholanzi.

Wajumbe wengine wa Jopo ni Marais wa nchi za Afrika Kusini, Tanzania, Kenya, Gambia, na DRO pamoja na Mfalme wa Morocco.

Rais Mstaafu Mhe. Kikwete ni Mwenyekiti Mwenza Msaidizi ambaye jukumu lake ni kuwasaidia Wenyeviti Wenza Watatu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mkutano ulifunguliwa na Mhe. Cyril Ramaphosa, Rais wa Afrika Kusini na Mwenyekiti wa G20 kwa mwaka 2025, na ulihudhuriwa na Mfalme Mswati wa Ill wa Eswatini, Mhe. Duma Boko, Rais wa Botswana na viongozi mbalimbali wa Kiserikali, Mashirika na wadau wa maji barani Afrika.

Katika hatua nyingine, Mhe. Kikwete ameteuliwa kuwa mmoja wa viongozi wakuu watano wa Baraza la Uwezeshaji wa Uenyekiti wa Afrika Kusini wa G20 kwa mwaka 2025 wakishughulikia masuala ya maji, na yeye akiwa Mwenyekiti Mwenza Msaidizi . Wengine ni Rais Sheikh Mohamed bin Zayed Al Nahyan wa Umoja wa Falme za Kiarabu (Co-Chair); Waziri Mkuu Mia Mottley wa Barbados (Co-Chair); Bw. Bill Gates, Mwenyekiti wa Mfuko wa Gates (Co-Chair); na Mhe. Amina J. Mohammed, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Mwaka huu nchi ya Afrika Kusini ni Mwenyekiti wa Kundi la Nchi 20 (The G20).

Mkutano huu wa Viongozi wa Afrika unataka Programu ya Uwekezaji wa Maji ya Afrika ipewe kipaumbele katika agenda za mkutano ujao wa G20 utakaofanyika Novemba 2025, Cape Town, Afrika Kusini.

# RC Mara awataka waratibu Siku ya Mto Mara kuwashirikisha wadau zaidi

Mkuu wa Mkoa wa Mara Mhe. Kanali Evans Alfred Mtambi amewataka waandaaji wa siku ya Bonde la Mto Mara kuongeza jitihada katika kuwashirikisha wadau kutoka Tanzania, na Kenya pamoja na wadau wa mendeleo ili kufanikisha utunzaji wa Bonde la Mto Mara.

Wito huo ameutoa alipomwakilisha Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) katika kufunga maadhimisho ya 14 ya Siku ya Mara yaliyofanyika mjini Butiama.

Amesema bonde la mto Mara lina umuhimu mkubwa kwa jamii ya Tanzania na Kenya inayozunguka bonde hilo hivyo njia mbalimbali zinatakiwa kutumika ili kufikia malengo.

Amepongeza jitihada ambazo zimekuwa zikifanyika zimesaidia kuendelea kuwepo kwa bonde hilo ambalo matokeo yake ni mto Mara ambao umechangia kuifanya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuwa moja ya Maajabu Saba ya Dunia.

Amesema jitihada hizo pia zilenge kuwa na Jukwaa la wadau wa Mto Mara na kufufua Jukwaa la Jumuia ya Watumia Maji ambalo linaweza kuweka utaratibu wa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka.

Amepongeza jitihada zinazoendelea ikiwemo kuanzisha mpango wa pamoja wa matumizi ya maji pamoja na hati ya makubaliano kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji ya Mto Mara.

Amesisitiza uanzishaji wa vikundi vya uhifadhi wa mazingira shuleni ili kuwajengea uelewa na utayari wa kulinda mazingira kuanzia ngazi ya shule.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji







Mhandisi Mwajuma Waziri ametoa salamu za Wizara ya Maji akieleza kuwa imeridhishwa na ushiriki wa wadau katika maadhimisho na imetumia fursa ya maadhimisho kufanya ukaguzi wa miradi ya maji ya Mugango-Kiabakari-Butiama, Mugumu-Seregenti na mradi wa maji wa Tarime-Rorya inayotekelezwa na Wizara ya Maji mkoani Mara.

Amewahakikishia wananchi wa Mkoa wa Mara kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mkoani hapo na anaendelea na jithada kuhakikisha lengo la “kumtua mama ndoo ya maji kichwani” linafanikiwa

# Mhandisi Mwajuma awataka Wahandisi kuchangamkia fursa za utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amewataka wahandisi nchini kuchangamkia fursa ya kufanikisha malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayolenga kulifikisha taifa katika uchumi wa kipato cha kati cha juu.

Amesema hayo akiwasilisha mada kuhusu 'Nafasi ya uhandisi katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050' katika Maadhimisho ya 22 ya siku ya Wahandisi Tanzania yenye kaulimbiu isemayo 'Wajibu wa Wahandisi kuelekea Dira ya Maendeleo 2050' jijini Dar es salaam.

Amesema kuwa sekta ya maji ni nguzo ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi na inahitaji ubunifu wa kihandisi ili kufanikisha miradi mikubwa kama ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji, mabwawa makubwa, na miundombinu ya umwagiliaji yenye ufanisi wa matumizi ya maji.

Amebainisha baadhi ya changamoto zinazohitaji mchango wa wahandisi katika sekta ya maji ikiwemo gharama kubwa za umeme kwenye miradi ya maji, uwezo mdogo wa ndani kujenga miradi mikubwa, na hitaji la viwanda vya ndani vinavyotengeneza dira za maji.

"Kuna fursa mpya za miradi tasnia ya Uhandisi inaweza kutekeleza:- Decentralized




Smart Water System, Solar-Powered Desalination for Coastal and Island Communities, Wastewater to Resource Solution and Flood Resilience Engineering." Mhandisi Mwajuma Amesema.

Amesisitiza kuwa Wizara ya Maji imeshaanza utekelezaji wa ujenzi wa gridi ya Taifa ya maji ambapo miradi mikubwa ya maji imetekelezwa na inaendelea kutekelezwa katika maeneo yenye maji ya uhakika kama vile maziwa, mito, na mabwawa makubwa hivyo wahandisi wanaweza kushiriki katika kufanikisha maendeleo zaidi.

Ameongeza kuwa maji ni sekta wezeshi na ni kichocheo na nyenzo ya mageuzi na imepewa



uzito katika kufanikisha dira ya Taifa ya 2050, kuwa na taifa lenye lenye uhakika na usalama wa maji kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

# Hungary kushirikiana na Tanzania mradi wa maji wa Biharamulo

Tanzania imefanya majadiliano na nchi ya Hungary ili kufanikisha utekelezaji wa mradi wa maji wa Biharamulo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Mahomud Thabit Kombo ameongoza majadiliano hayo yaliyohusu mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Hungary kwa lengo la kutekeleza Mradi wa Usambazaji Maji wa Biharamulo.



Majadiliano yamefanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki jijini Dar es Salaam kati ya serikali ya Tanzania pamoja na ujumbe kutoka Hungary ukiongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Biashara wa nchi hiyo Mhe. Peter Szijjarto.

Mhe. Kombo amesema mradi huo ni sehemu ya jitihada za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha jamii ya inaondokana na uhaba wa huduma ya majisafi na salama.



Amesema mradi huo unategemea kutumia teknolojia za kisasa za kusafirisha maji kutoka ziwa Victoria na kuyatibu kabla ya kufikisha kwa wananchi.

Naye Mhe. Peter Szijjarto amesema serikali ya Tanzania imekuwa mshirika mzuri wa maendeleo na serikali ya Hungary. Amesema uhusiano huo ndio umewezesha kuleta mradi huo wa masharti nafuu kwa usalama wa afya ya wananchi na Afrika kwa ujumla.

Ziara ya Waziri Szijjarto pamoja na majadiliano kuhusu sekta ya maji inalenga kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia na kiuchumi baina ya Tanzania na Hungary

# Katibu Mkuu Maji aweka kambi Butimba kwa saa 24 kuhakikisha huduma ya maji inarejea Mwanza.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amefika katika mradi wa maji wa Butimba kufuatilia marekebisho yanayoendelea ili kurejesha huduma ya maji katika hali ya kawaida kutokana na hitilafu iliyotokea katika mtambo wa kusukuma maji.

Mhandisi Mwajuma amefanya kazi kwa saa 24 na wataalam katika kurekebisha hitilafu iliyojitokeza kwa lengo la kuhakikisha maji yanapatikana kwa wananchi muda wote kutokana na uwekezaji mkubwa wa serikali katika mradi wa maji wa Butimba.







# Sekta ya maji yapongezwa kwa ushirikiano na asasi ya kimataifa ya maji

Sekta ya Maji imepongezwa kwa ushirikiano na Asasi ya kimataifa ya maji, pamoja na utekelezaji wa miradi ya maji.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Arusha Mjini Dkt. Jacob Rombo, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo amesema hayo wakati wa mafunzo ya watumishi wanaohusika na usanifu wa miradi ya maji jijini Arusha.

Ameipongeza serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uwekezaji mkubwa na kazi zinazoonekana kupitia matokeo ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

Dkt. Shauku Kihombo, Mratibu wa Ushirikiano wa RUWASA amesema ushirikiano unaendelea na wadau mbalimbali wa Maendeleo wa ndani na nje ya nchi katika maeneo ya Ujenzi, Usimamizi wa Miradi na Mafunzo ili kutimiza azma ya serikali kufanikisha wakala na taasisi za umma kushikiriana na wadau wake katika kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali na kuwezesha wananchi kupata huduma muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Naye mwakilishi kutoka, Asasi ya Dunia ya Maji, Bi. Alyson Rockland pamoja na Bwn. Kogi Chege wameishukuru Wizara ya Maji na RUWASA kwa ushirikiano wanaopata katika kutekeleza majukumu yanayohusu huduma ya maji.






# Katibu Mkuu Maji asisitiza utoaji wa elimu ya utunzaji mto mara kwa wanafunzi



Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri ametoa wito kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kusisitiza utoaji wa elimu kwa wanafunzi ili kuwezesha elimu endelevu ya utunzaji wa mazingira ya Bonde la Mto Mara. Wito huo ameutoa Mjini Butiama akizindua maadhimisho ya Siku ya Mto Mara 2025.

Ameitaka jamii kushirikiana katika kudhibiti uvuvi haramu na uchafuzi wa maji ili kuulinda na kuuendeleza Mto Mara ambao ni tegemeo kubwa la maji ya kunywa kwa binadamu, kilimo, wanyama, uvuvi na shughuli nyingine za kijamii na uchumi.

“Tunahitaji kuhakikisha kuwa kila mtu anakuwa mlinzi wa Mto Mara kuanzia mtoto wa shule hadi mfugaji na mkulima. Tuimarishe elimu ya uhifadhi kwa wanafunzi shuleni, tuhimize matumizi endelevu ya ardhi, tushirikiane kudhibiti uvuvi haramu na uchafuzi wa maji, na tuwe mstari wa mbele kuripoti uharibifu wa mazingira.” Amesema Mhandisi Mwajuma

Amesisitiza kuwa Mto Mara ni chanzo cha maisha kwa maelfu ya watu na viumbe hai. Uharibifu wa Mto Mara ni kujiangamiza. Kuhifadhi Mto Mara ni kuhifadhi maisha ya sasa na ya baadae.

Amesema ziko baadhi ya baadhi ya changamoto kubwa zinazoukabili Mto Mara ni pamoja na uharibifu wa misitu kandokando ya mto, uchimbaji wa madini usiozingatia sheria, pamoja na uchafuzi wa maji unaotokana na shughuli za kibinadamu hivyo ushirikiano kati ya serikali, Jamii, Asasi za Kiraia, na Wadau wa Kimataifa, kutawezesha kugeuza changamoto hizi kuwa fursa na kupata mafanikio.

Ameongeza kuwa maadhimisho ya siku ya Mto Mara ambayo hufanyika kila mwaka Septemba 15 ni tukio lenye fahari kubwa kwani linatoa fursa ya kutafakari juu ya umuhimu wa Mto Mara unaotiririka kutoka milima ya Mau nchini Kenya kupitia Hifadhi za Masai-Mara na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na hatimaye kuingia Ziwa Victoria.



Maadhimisho ya Siku ya Mto Mara mwaka 2025 yanakwenda na kaulimbiu isemayo “Hifadhi Mto Mara. Linda Uhai”

# Serikali yalipa fidia ya shilingi milioni 999 kwa Wananchi 103 wa Dodoma kwa miradi ya maji

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Maji, imekamilisha zoezi la ulipaji wa fidia kiasi cha Shilingi Milioni 999 kwa wananchi 103 ambao ardhi yao ilitwaliwa katika maeneo ya Nzuguni, Zuzu Nala, Nala Chihoni na Kibaigwa kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya maji inayotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA).

Ulipaji wa fidia hizo, umeongozwa na Wizara ya Maji kwa kushirikiana na DUWASA, Wizara ya Ardhi na Viongozi wa Serikali za Mitaa wa maeneo husika, ambapo kwa eneo la Nzuguni, Wananchi 24 wamelipwa fidia ya Shilingi Milioni 148 tarehe 07 Agosti, 2025, Zuzu Nala Wananchi 51 ambao wamelipwa fidia ya Shilingi Milioni 594 tarehe 11 Agosti 2025, Nala Chihoni Wananchi 7 ambao walilipwa fidia yao ya Shilingi Milioni 58 tangu mwezi Aprili, 2025 na Kanda ya Kibaigwa Wananchi 23 wamelipwa fidia ya Shilingi Milioni 197 na kukamilisha zoezi hilo Agosti 12, 2025.





Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoa kiasi hicho cha fedha kwa wananchi waliotoa ardhi yao kupisha utekelezaji wa miradi ya maji.

“DUWASA, kwa niaba ya Wananchi wa maeneo ya Nzuguni, Zuzu Nala, Nala Chihoni na Kibaigwa, inaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita na Wizara ya Maji kwa juhudi zao kubwa na ufanisi katika kuhakikisha ulipaji wa fidia kwa wakati kwa wananchi wetu,” alisema Mhandisi Aron.

“Hatua hii ni muhimu sana kwa maeneo yaliyotekelezwa na yanayoendelea na utekelezaji wa miradi ya maji ya kimkakati katika Jiji la Dodoma na Kanda ya Kibaigwa, hii inaonesha dhamira ya Serikali katika kulinda haki za wananchi wakati wa kutekeleza miradi ya maendeleo.” Mhandisi Aron amesema.

Kwa upande wa wakazi wa Kibaigwa, Bi. Josephina Paulo ameishukuru serikali kwa kuwasikiliza na kuwalipa fidia. Ameiomba serikali kuwafikia wengine ambao bado hawajalipwa.

Naye Bwan Yohana Mwarabu ameshukuru serikali kwa malipo hayo.

# Wizara ya maji yaanza maandalizi ya awamu ya pili ya mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji




Menejimenti ya Wizara imekutana na wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ili kujadili maeneo ya kipaumbele katika Awamu ya Pili ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI II).

Awamu ya kwanza ya mpango huo inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba 2025, na Serikali imeanza maandalizi ya awamu inayofuata kwa lengo la kuboresha zaidi mazingira ya uwekezaji na biashara nchini.

Menejimenti ya Wizara ikiongozwa na Naibu Katibu Mkuu Bi. Dianna Kimario pamoja na wakuu wa Taasisi hizo zitafanya kikao kazi na Timu ya kitaifa ya Wataalam walioundwa kwa ajili ya maandalizi ya MKUMBI II itaendelea na kikao hicho ambacho kitajikita kwenye maeneo ya kipaumbele katika Sekta ya Maji na kukusanya taarifa muhimu zitakazosaidia katika uandaaji wa mpango huo.



# Matumizi ya Mfumo yapongezwa kwa kuleta mageuzi

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA kutoka Wizara ya Maji, Joash Nyitambe, ameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma (KUWASA) kwa hatua kubwa ya kutumia mfumo wa kidigitali wa kuripoti mivujo ujulikanao kama Amanzi (Amanzi App). Mfumo huu umetajwa kuwa chachu ya mageuzi katika Sekta ya Maji, ukisaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza na kudhibiti upotevu wa maji.

Akizungumza mjini Kigoma, Nyitambe amesema kuwa hatua ya KUWASA kutumia teknolojia katika kusimamia huduma za maji ni mfano bora wa kuigwa na mamlaka nyingine kote nchini.

"Tunajivunia kuona teknolojia ikitumika kuboresha huduma na kutatua changamoto za wananchi. Hongereni sana kwa hatua kubwa hii ya kiubunifu ambayo inagusa moja kwa moja maisha ya wananchi," Nyitambe amesema.

Katika ziara hiyo, Nyitambe alipata fursa ya kutembelea maeneo kadhaa na kujionea namna mfumo wa Amanzi unavyofanya kazi kwa ufanisi. Alisisitiza kwamba matumizi ya teknolojia bora kama huu si tu yanarahisisha huduma, bali pia yanathibitisha kuwa sekta ya maji inaweza kuwa kinara katika uvumbuzi na matumizi ya TEHAMA kwa manufaa ya jamii.

Amanzi ni mfumo maalum wa kuripoti mivujo uliobuniwa na Kampuni ya Collect Tech. Mfumo huu unafanya kazi kwa namna , ambapo mwananchi anapobaini mvujo katika eneo lolote, anaweza kutoa taarifa papo hapo kupitia simu yake ya mkononi.




Baada ya taarifa hiyo kupokelewa na mfumo, mafundi wa KUWASA hukimbilia eneo husika kwa haraka na kuchukua hatua za kudhibiti mvujo huo. Utaratibu huu umeleta mapinduzi makubwa kwa kuokoa maji yaliyokuwa yanapotea bila sababu, na hivyo kuongeza ufanisi wa usambazaji maji kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Nyitambe, mfumo huo ni ushahidi tosha kwamba matumizi sahihi ya teknolojia yanaweza kuleta mabadiliko chanya, kuongeza uwajibikaji, na kuhakikisha huduma za maji zinatolewa kwa ubora wa hali ya juu. Aliitaka KUWASA kuendelea kusimamia vizuri mfumo huu na akazitaka mamlaka nyingine nchini kuiga mfano huo kwa ajili ya manufaa ya wananchi.

Mfumo huu umeundwa si kwa ajili ya KUWASA pekee, bali pia kwa kushirikisha wananchi moja kwa moja katika kulinda rasilimali ya maji. Kupitia Mfumo wa Amanzi, kila mmoja ana nafasi ya kushiriki katika kutunza rasimali maji.

Serikali imesaidi mkataba wa kuimarisha huduma ya maji katika mji wa Nachingwea. Mkataba huo unalenga kuhakikisha huduma ya maji kwa wananchi inaongezeka na kuwa imara zaidi. Pichani ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisasi na Usafi wa Mazingira Masasi – Nachingwea (MANAWASA) Bw. Kiula Kingu akishiriki katika hafla hiyo






# Mafunzo ya tahadhari kwa mabwawa kufanyika Mwanza







Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Chemba ya Migodi Tanzania pamoja na watalaam wa Kampuni ya Uhandisi ya City wameshirikiana kuandaa mafunzo ya siku tatu (3) yatakayoshirikisha wataalam kutoka Sekta Binafsi na Serikalini ikiwamo wamiliki wa migodi kwa ajili ya usalama wa mabwawa ya majisafi na tope sumu (TSF).

Mafunzo yatafanyika jijini Mwanza kuanzia Novemba 19-21, 2025 yakiwa na kaulimbiu isemayo 'Tahadhari za dharura za Kukabiliana na Majanga ya Mabwawa ya Maji na Tope sumu' .

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Maji Diana Kimario ambaye pia ni Mkurugenzi Tathmini na Ufuatiliaji akiongea na vyombo vya habari Mtumba jijini Dodoma amesema mafunzo hayo hufanyika kila mwaka na mwaka 2025 ni mara ya tatu mfululizo ambapo mafunzo yamekuwa na mchango chanya katika kujenga uelewa wa namna bora ya kukabiliana na matatizo yanayotokana na mabwawa yakiwemo mabwawa ya tope sumu.

Aidha mafunzo hayo yamekuwa yakijumuisha wataalam waliobobea kutoka mataifa yaliyoendelea kwenye eneo linalohusu usalama wa mabwawa jambo ambalo limewezesha ufanisi wa mabwawa na kuepusha changamoto zinazosababishwa na mabwawa.

Amesisitiza kuwa Serikali chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inaamini katika ushirikishwaji wa wadau wa sekta binafsi hivyo Wizara ya Maji itaendelea kuwa karibu na wadau hao ili kuhakikisha malengo yanafikiwa.

Amewataka wadau wote wa mabwawa ndani na nje ya nchi kujitokeza kujiandikisha ili kushiriki mafunzo hayo.

Mtendaji Mkuu wa Chemba ya Migodi Tanzania (Tanzania Chamber of Mines-TCM) Benjamini Mchwampaka ameipongeza serikali kwa jinsi ambavyo imekuwa ikitoa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu. Amesema wataendeela kuwa pamoja ili kuhakikisha sekta ya maji na madini kwa ujumla zinakuwa na kuifikia jamii.

Waziri wa Maji, Usafi wa Mazingira na Umwagiliaji wa Jamhuri ya Kenya Mhe. Erick Mugaa pamoja na ujumbe wake wakipokelewa katika uwanja wa Mwenge mjini Butiama katika Kilele cha maadhimisho ya 14 ya Siku ya mto Mara 2025.
Maadhimisho ya Siku ya Mara yanafanyika kila mwaka yakilenga kushirikishana njia mbalimbali za kuwezesha, kulinda, kutunza na kuendeleza Bonde la Mto Mara ambalo lina mchango mkubwa wa kuifanya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa upande wa Tanzania na Hifadhi ya Maasai Mara upande wa Kenya kuwa kivutio kikubwa cha utalii



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Suleiman Serera ametoa pongezi kwa Wizara ya Maji kwa kazi kubwa ya kufikisha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi, mijini na vijijini.
Dkt. Serera amesema Sekta ya Maji imeimarika kwa kiasi kikubwa na kuwa chachu ya maendeleo nchini, akisisitiza uongozi umeshikama na wataalam.
Dkt. Serera ametoa pongezi hizo wakati akiwa kwenye Banda la Wizara ya Maji, na kuzungumza na wataalam wa Sekta ya Maji katika Maonesho ya Nanenane katika Viwanja vya Nzuguni, Jijini Dodoma.



# Wizara ya Maji imeandaa warsha inayohusu mikakati ya Sekta ya Maji katika kufanikisha mchango wa kitaifa wa kukabiliaba na mabadiliḳo ya tabianchi.

Warsha hiyo imefanyika jijini Dodoma na ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha sekta ya maji inatatua changamoto zinazoikabili ikiwemo kupambana na mabadiliko ya tabianchi ili kuwezesha upatikanaji wa huduma endelevu ya maji kwa matumizi mbalimbali katika kijamii.

Warsha imewahusisha wataalamu kutoka sekta ya maji, Wadau wa Maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi pamoja na wizara za Kisekta.

Wajumbe wa Warsha wamejikita kujadili kwa kina mbinu, miongozo na njia muafaka za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



# Katibu Mkuu Maji asisitiza utoaji wa elimu ya utunzaji mto mara kwa wanafunzi

Maadhimisho ya 14 ya Siku ya Mara yameendelea kuipa heshima Sekta ya Maji kwa kuwatunuku Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri pamoja na Wizara ya Maji kwa ujumla.

Viongozi hao wamepewa tuzo na kutajwa kama kielelezo cha utendaji bora ambao umewezesha mafanikio makubwa katika Sekta ya Maji nchini Tanzania.





Jarida Tando



**Kitengo cha Mawasiliano**

Tovuti: www.maji.go.tz